

14C-Nuwn Saakinah Na Tanwiyn -Iqlaab - Kugeuza

iii- الإِفْلَابُ Al-Iqlaab - Kugeuza

Maana yake ni kugeuza kitu na kinavyotakiwa kuwa au kupindua kitu. Katika hukmu za Tajwiyd ni kuigeuza nuwn saakinah au tanwiyn kwa kuitamka kama ni م (miym) pamoja na kuleta ghunnah na pia kuleta إِحْفَاءِ الْشَّفَوِيِّ (ikhfaa shafawiy). Hukmu hii hutokea pale tanween au nuwn saakinah inapofuatiwa na herufi moja tu nayo ni ya ب (baa).

Iqlaab inaweza kutokea katika neno moja au maneno mawili.

Katika Misahafu aghlabu hukmu hii imebainishwa kwa kuwekwa م (miym) ndogo juu ya nuwn.

Iqlaab katika nuwn saakinah			
Katika maneno mawili		Katika neno moja	
Inavyotamkwa	Mfano	Inavyotamkwa	Mfano
mim mm -ba'di	مِنْ بَعْدِ	layu mm -badhanna	لَيْتَبَذَّنَ
ma mm -bakhila	مَنْ بَخَلَ	am mm -biuwniy	أَنْبَعْوَنِي
am mm -buwrika	أَنْ بُورِكَ	fam mm -bajasat	فَانْجَسَّتْ
mi mm -ba'dhwin	مِنْ بَعْضٍ	yu mm -bitu	يُنِيتُ

Iqlaab katika tanwiyn

Inavyotamkwa	Mfano	Inavyotamkwa	Mfano
Samiy'amm-Baswiyyraa	سَمِيعًا بَصِيرًا	'utullimm-ba'da	عُتُلْ بَعْدَ
'Aliymumm-bidhaati	عَلِيمٌ بِذَاتِ	aayaatimm-bayyinaatin	ءَايَتٍ بِبَيِّنَاتٍ